**Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.**

Budget Documents Government Budget Speeches

1982-06-17

# Hotuba ya Waziri wa Fedha Mh.A.H Jamal (Mb) akiwasilisha bungeni mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 1982-83

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara ya Fedha

https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/677

*Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# Hotuba ya Waziri wa Fedha, Ndugu A. H. Jamal, Mbunge, akiwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 1982/83 tarehe 17 Juni, 1982

1982
KIMEPIGWA CHAPA NA MPIGACHAPA WA SERIKALI
DAR ES SALAAM—TANZANIA

# HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA, NDUGU A. H. JAMAL, MBUNGE, KWENYE BUNGETAREHE 17 JUNI, 1982 AKIWASILISHA BUNGENI MAPENDEKEZO YA SERIKALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA 1982/83

Ndugu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa likae kama Kamati ya Matumizi ili lijadili na hapo baadaye kuidhinisha mapendekezo ya Serikali kuhusu Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 1982/83.

2. Ndugu Spika, leo asubuhi Bunge lako Tukufu limesikia, kutoka kwa Waziri Prof. Malima, maelezo kuhusu hali ya uchumi wa Taifa ilivyo mbaya. Hatuwezi kujiridhisha na hali hii wala kudhania kuwa hali hii itabadilika yenyewe. Kwa kipindi cha muda mrefu ujao tutaendelea kuwa na hali hii ngumu. Mwaka jana, mwanzoni mwa hotuba yangu ya bajeti nilieleza kuwa "Inatupasa kugawa rasilimali ndogo tuliyonayo kwa makini zaidi ili tuweze kuendeleza shughuli za kijamii na kiuchumi tulizonazo sasa na kuchagua kwa uangalifu mkubwa miradi ya maendeleo ambayo itapunguza au kuondoa kabisa vikwazo ambavyo vinatufanya tusiweze kutumia kikamilifu vitega uchumi vilivyopo kufikia kiwango cha uwezo wetu".

3. Ni jukumu la Ndugu Wabunge, kuamua kama kweli tumefanikiwa kuzingatia utaratibu huu kwa kiwango kilichotegemewa. Nionavyo mimi wakati huu hatuna njia nyingine bali tukubali uwezekano wa kufunga baadhi ya shughuli za uzalishaji ili tuweze kutumia rasilimali ndogo tuliyonayo vizuri zaidi katika sekta zitakazobaki.

4. Kwa kuwa hatuna uwezo juu ya mazingira ya nje, ambayo yanazidi kutugandamiza, tumaini letu kubwa kwa siku za usoni liko katika uwezo na juhudi zetu wenyewe katika kuujenga uchumi wetu. Hata hivyo, haitoshi kusema hivyo tu bali kuna haja ya kuonyesha kwa vitendo, kila

wakati, tabia, nia na uwezo wa kutumia kidogo tulichonacho kwa uangalifu mkubwa, kubana matumizi yetu na kuwa na tabia ya kujinyima kwa ajili ya kujenga uchumi imara kwa siku za usoni.

**Matokeo ya Hesabu za Serikali za mwaka 1980/81:**

5. Ndugu Spika, wakati wa kufunga Hesabu za mwaka wa fedha 1980/81 hali ilikuwa kama ifuatavyo:—

Makadirio ya matumizi yaliyoidhinishwa ikiwa ni pamoja na matumizi ya nyongeza Sh. 16,452.4m.

| | Sh.<br>Sh. |
|---|---|
| Matumizi Halisi ........................................ | 14,802·4m |
| Matumizi ya Kawaida ................................ | 10,045·9m |
| Matumizi ya Maendeleo ............................ | 4,756·5m |
| Makadirio ya Mapato ................................ | 14,248·1 m |
| Mapato halisi .......................................... | 12,295·1 m |
| Mapato ya Kawaida .................................. | 8,795m |
| Mapato ya Maendeleo ................................ | 3,500·1m |
| Makadirio ya Mikopo ya Serikali toka benki | 2,204·3m |
| Mikopo halisi ya Serikali kutoka benki ..... | 3,009m |

Ujazi wa fedha uliongezeka kwa asilimia 26.5 ukilinganisha na kadirio la asilimia 18.5 mwanzoni mwa mwaka wa fedha 1980/81.

**Mwenendo wa Fedha pamoja na Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 1981—82:**

6. Ndugu Spika, itakumbukwa kwamba makadirio ya matumizi ya kawaida yaliyoidhinishwa na Bunge yalikuwa Sh. 12,205·4m/-. Inavyoelekea, hivi sasa, matumizi ya kawaida mwishoni mwa mwaka huu wa fedha, yatafikia Sh. 13,687 milioni. Wizara, Mikoa na Idara zifuatazo zilivuka viwango vya makadirio ya matumizi yaliyoidhinishwa:— Ngome, Usalama, Kaziustawi, Mifugo, Arusha, Pwani, Dodoma, Iringa, Kilimanjaro, Lindi, Mara, Mbeya,

Morogoro, Mwanza, Ruvuma, Shinyanga, Singida, Tanga na Kagera. Vile vile mashirika mengi ya umma hasa mamlaka za mazao, kutokana na matatizo mbali mbali, yalibidi kuomba fedha Hazina kwa ajili ya shughuli zao, kwa kiasi ambacho ama kilikuwa hakikutengwa au kilizidi kiwango kilichotengwa katika bajeti. Maombi ya fedha za nyongeza (Supplementary Estimates) yataletwa kwa ajili hii.

7. Kwa upande wa mapato, tunatarajia kukusanya Sh. 10,460 milioni ukilinganisha na makadirio ya Sh. 10,681 milioni na hivyo tunakuwa na upungufu wa Sh. 221 milioni. Makadirio ya mapato kutoka ushuru wa forodha yalikuwa Sh. 1,020 milioni ambapo mapato halisi yanatarajiwa kuwa Sh. 580 milioni yakiwa na upungufu wa Sh. 440 milioni. Upungufu huu unatokana na uhaba wa fedha za kigeni ambao umelazimu taifa kupunguza sana uagizaji wa bidhaa kutoka nje jambo ambalo lilifanya ushuru wa forodha pia kupungua. Kodi ya mauzo ilikuwa imekadiriwa kuwa Sh. 5,409 milioni ingawa sasa inatarajiwa kuwa makusanyo halisi hadi mwisho wa mwaka huu yatakuwa Sh. 4,700 milioni ikiwa ni upungufu wa Sh. 709 milioni. Upungufu huu ulisababishwa na kushuka kwa uzalishaji katika viwanda kutokana na viwanda kushindwa kutumia uwezo wao wa kuzalisha kikamilifu kutokana na uhaba wa malighafi, ukosefu wa spea, na uharibikaji wa mashine wa mara kwa mara. Kwa upande wa kodi ya mapato, ilikuwa imekadiriwa kuwa makusanyo yangefikia Sh. 1,764·0 milioni lakini sasa inatarajiwa kuwa makusanyo yatafika Sh. 2,800·0 milioni ikiwa na ongezeko la Sh. 1,036·0 milioni. Ongezeko hili linatokana na ongezeko la ufanisi katika ukusanyaji unaofanywa na Idara ya Kodi ya Mapato.

8. Kama ilivyotamkwa na Ndugu Waziri wa Uchumi na Mipango katika Ofisi ya Makamu wa Rais, mapato kwa ajili ya maendeleo yanatarajiwa kuwa Sh. 3,825 milioni ukilinganisha na makadirio ya Sh. 5,297 milioni. Matumizi kwa ajili ya maendeleo yanatarajiwa kufika Sh. 5,000 milioni ukilinganisha na makadirio ya Sh. 6,622 milioni.

9. Kwa pamoja, jumla ya mapato yote ikiwa ni mapato ya kawaida na ya maendeleo yanakadiriwa kufikia Sh. 14,285 milioni. Vile vile jumla ya matumizi yote ikiwa ni matumizi ya kawaida na ya maendeleo yatafikia Sh. 18,687 milioni. Mikopo ya Serikali kutoka mabenki itakuwa Sh. 4,402 milioni. Hivyo ujazi wa fedha ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha utakuwa karibu asilimia 25 ikilinganishwa na kiasi cha asilimia 20 kilichokadiriwa hapo awali.

10. Hali hii inatia wasi wasi. Kwa upande wa mapato, makusanyo ya kodi ya mapato yalizidi makadirio ya mwaka na hivyo hatuna budi kuipongeza Idara ya Kodi ya Mapato kwa kazi hii, ingawa wakati huo huo itabidi kwa siku za usoni tuhakikishe kuwa makadirio yanatayarishwa kwa uangalifu zaidi. Kwa bahati mbaya makusanyo ya mauzo na ushuru wa forodha hayakuweza kufikia malengo yaliyowekwa. Kwa hiyo, kwa jumla mapato yalipungua kwa Sh. 221 milioni.

11. Kuhusu matumizi ya kawaida, inaridhisha kuona kuwa Wizara nyingi zilijitahidi kwa dhati na kufanikiwa kutovuka viwango vilivyowekwa. Hii inaonyesha kwamba Wizara na Mikoa ambayo ilivuka viwango vilivyo idhinishwa, ingeweza kusaidia katika vita vya kupambana na ongezeko la bei kama ingeonyesha jitihada na uangalifu katika usimamizi wa matumizi ya fedha kama ilivyofanywa na Wizara nyingine za Serikali.

12. Hali yetu ya fedha za kigeni iliendelea kuwa ngumu sana. Malimbikizo ya madeni yetu yanayotokana na biashara ya nje yanatazamiwa kufikia Sh. 3,020 milioni ukilinganisha na malimbikizo ya Sh. 2,449 milioni mwanzoni mwa mwaka. Bei za mazao tunayouza nje ziliendelea kudidimia wakati riba za mikopo ziliendelea kupanda na hivyo kufanya pato la fedha za kigeni ambalo tungelitumia kwa kuagizia mahitaji ya lazima kuwa dogo. Kwa mfano ongezeko la asilimia moja katika riba linabebesha nchi zinazoendelea mzigo wa kulipia mikopo yao kwa dola 1·5 bilioni kila mwaka. Katika hali hii ilitulazimu tuendelee kujinyima vitu muhimu ambavyo tulipashwa kuviagiza kwa ajili ya kuendesha uchumi wetu.

13. Viwango vya juu vya riba na mabadiliko ya mara kwa mara ya thamani ya sarafu zinazotumika zaidi katika shughuli za biashara duniani, yaliifanya thamani ya fedha yetu, ukilinganisha na fedha za nchi nyingine, iongezeke visivyo. Ni wazi kuwa ongezeko la aina hii katika thamani ya fedha yetu linaathiri uchumi wetu. Kwa ushauri wa Benki Kuu tulishusha thamani ya shilingi kwa kiasi cha asilimia 10—12 kwa thamani ya dola ya Marekani. Hii italeta ongezeko la mapato katika shilingi kwa bidhaa tunazouza nje na pia kuongeza kidogo gharama za kununulia bidhaa kutoka nje kutegemea uwezo wetu wa kuagiza bidhaa hizo kutoka nje. Katika hali hii ya wasi wasi kuhusu viwango vya riba na thamani ya fedha duniani, usimamizi wa thamani ya fedha yetu unazidi kuwa mgumu na utahitaji uangalifu mkubwa zaidi.

14. Kama Ndugu Wabunge wanavyofahamu hadi hivi majuzi asilimia saba ya mapato yatokanayo na mauzo yetu ya nje ilikuwa inatumika kulipia madeni ya nje. Hali hii sasa imebadilika sana licha ya nchi rafiki kutustahi na kufutilia mbali madeni ya muda mrefu waliyokuwa wanatudai. Baadhi ya sababu za kuongezeka kwa malipo ni zifuatazo: Kwanza, riba inayotozwa na Mabenki ya Biashara ya nje katika ununuzi wa bidhaa imepanda sana kufuatana na vurugu ya hali ya fedha duniani. Pili hivi sasa tunaingia katika kipindi ambapo madeni yasiyo ya muda mrefu yanaanza kulipwa mbali ya malipo yanayofanyika kuhusu mikataba mbali mbali ya muda mfupi. Tatu, mkopo mkubwa tuliopata kutoka Jamhuri ya Watu wa China kwa ajili ya kujengea Reli ya Uhuru utaanza kulipwa kuanzia mwaka ujao wa fedha. Kutokana na taarifa za Benki Kuu gharama za kulipia madeni ya nje zitaongezeka sasa hadi kufikia asilimia 19 ya mategemeo ya mapato ya mauzo yetu ya nje. Pamoja na mahitaji yetu ya mafuta yanayotarajia kuchukua asilimia 50 ya mapato ya mauzo ya bidhaa zetu nje, ni dhahiri kwamba kiasi kinachobaki ni kidogo mno kutosheleza uagizaji wa angalau vitu vichache ambavyo ni muhimu sana kwa mahitaji ya Taifa.

**Mpango wa Kurekebisha Hali ya Uchumi:**

15. Ndugu Spika, ni katika kuelewa hali hii ngumu, tunapaswa kutafakari kikamilifu maelezo yaliyotolewa na Waziri Prof. Malima kuhusu uamuzi wa Serikali wa kuwa na mpango wa kudumu wa kurekebisha hali ya uchumi, mpango ambao unatupa upeo wa muda mrefu wa mpango wetu wa kujihami kiuchumi. Kwa hiyo, itabidi tuendelee na mpango wa kujihami kiuchumi mwaka hadi mwaka kwa kuzingatia misingi na malengo ya mpango wa kudumu wa kurekebisha uchumi. Ni muhimu kabisa kuwa sisi sote tuelewe malengo na shabaha za mpango huu. Ikiwa mwishoni mwa mpango huu itadhihirika kuwa tumeshindwa kufanya marekebisho ambayo yangetufanya tuongeze ufanisi na tija katika shughuli zetu za uzalishaji na uuzaji katika masoko ya nje, na pia usambazaji wa bidhaa na huduma hapa nchini, ni dhahiri kwamba juhudi zetu zitakuwa zimeshindwa, na tutakuwa tumeachia watakaotufuata na vizazi vilivyo kazi ngumu ya kurekebisha uchumi wa nchi.

16. Kuhusu shughuli za usimamizi wa fedha na suala zima la mwenendo wa fedha na sera inayohitajiwa kuratibu na kurekebisha mwenendo huu, serikali itawajibika kuchukua uamuzi katika sehemu muhimu zifuatazo:—

**Riba:**

17. Benki Kuu itategemewa kuchambua kwa makini, mara kwa mara viwango vya riba, kuliko ilivyokuwa hapo awali, kwa madhumuni ya kutoa motisha wa kutosha kwa waweka akiba na hasa wale wa viwango vidogo na huku kuwafanya wakopaji watambue gharama halisi ya fedha. Katika mazingira ya kupanda kwa bei haraka haraka kazi hii siyo rahisi. Hata hivyo ni kwa sababu hiyo hiyo inakuwa lazima tuweke juhudi zetu zote katika kukabili hali hii.

18. Kwa kuwa viwango vya riba vinaonyesha gharama ya kutumia fedha, liwe ni jukumu letu sote kuhakikisha kwamba wasimamizi wetu wa fedha wanatekeleza wajibu wao kwa kuzingatia gharama hii katika kusimamia shughuli

zao. Ni katika kutekeleza wajibu huu, ndipo Mameneja wa Mashirika ya Umma wanaweza kuepukana na lawama za kuwa ni wafujaji mali, sio waangalifu kuhusu gharama za kuendesha mashirika yao, iwe ni kununua malighafi, usafiri au buduma nyinginezo au gharama ya fedha yenyewe. Meneja wa Fedha anayefanya kazi kwa kuzingatia kiwango cha mkopo aliorubusiwa na benki, kiwango ambacho kinatolewa baada ya kuchambua kwa uangalifu mahitaji ya kuendesha shughuli za shirika, atakuwa amechangia kikamilifu katika uimarishaji wa uchumi wa taifa. Meneja wa Fedha ambaye hajali kuelewa athari za kutobeshimu viwango vya karadha/mikopo alivyopangiwa, anabatarisha uchumi wa taifa hili.

**Gharama za Uendeshaji katika Mashirika ya Umma:**

19. Ndugu Spika, gharama za uendeshaji katika mashirika ya umma ni suala ambalo linaipa Serikali wasi wasi mkubwa. Katika kukabili hali hii isiyoridhisha, Wizara Mama zote zimetakiwa kuyaagiza Mashirika yote yaliyo chini yao kuhakikisha kuwa gharama za uendeshaji hazizidi viwango vya mwaka uliopita na kiasi kitakachopunguzwa kiwekwe kwenye akaunti maalum na hatimaye fedha hiyo ilipwe Hazina. Kila Sbirika la Umma linatakiwa kutoa taarifa ya akaunti hii Hazina ifikapo mwisho wa Septemba 1982.

## MASHIRIKA YA FEDHA

20. Ndugu Spika, sasa nitazungumzia, kwa muhtasari, Mashirika ya Fedha.

**Benki Kuu:**

21. Ndugu Spika, mwaka jana katika hotuba yangu ya bajeti nilitaja kuwa upungufu mkubwa wa fedha za kigeni uliokuwa unakabili Taifa uliathiri uwezo wa Benki Kuu katika kutekeleza wajibu wake vizuri. Hali ya fedha za kigeni iliendelea kuwa mbaya mwaka uliopita na hivyo kuzidi

kuathiri uwezo wa Benki wa kutekeleza wajibu wake. Hata hivyo, pamoja na matatizo haya, Benki ilijitahidi kadri ilivyoweza kugawa kiasi kidogo cha fedha za kigeni kilichokuwepo kwa ajili ya mahitaji mubimu.

22. Benki Kuu imeendelea kukuza juhudi zake za kusukuma maendeleo vijijini kwa njia ya kutoa mikopo kwa mashirika ya fedha yanayohusika. Mfuko wa fedha wa maendeleo Vijijini ulifikia Sh. 173·1 milioni mwishoni mwa Juni 1981 ukilinganisha na shilingi 104·9 milioni mwishoni mwa Juni 1980. Katika kusaidia sekta nyingine za uchumi, Benki Kuu imo katika hatua ya kuanzisha mifuko mingine ambayo itahudumia sekta ya viwanda hasa viwanda vidogo kwa madhumuni ya kutoa dhamana kwa mikopo itolewayo na mashirika ya fedha kwa viwanda hivi. Kwa upande wa maendeleo vijijini, uwezekano wa kuwa na mfuko wa kupunguza riba kwa mikopo itolewayo na Benki ya Maendeleo Vijijini kwa ajili ya kujengea maghala vijijini unachunguzwa. Pia suala la kutoa motisha kwa wauzaji bidhaa nje linatazamwa kwa makini. Baada ya kukamilisha maandalizi haya, Benki Kuu itatangaza rasmi uanzishaji wa mifuko hii.

**Benki ya Taifa ya Biashara:**

23. Baada ya kipindi ambapo Benki ilipanuka kwa haraka kutoka matawi 44 na wafanyakazi 3,000 katika mwaka 1970 hadi kufikia matawi 109 na wafanyakazi 6,000 hivi sasa, ni dhahiri kwamba ipo haja ya kujizatiti zaidi. Ninafurahi kuona kwamba Uongozi wa Benki pamoja na Baraza la Wafanyakazi wanatambua umuhimu huu na wamekusudia kutimiza lengo hili katika kipindi cha miaka miwili hadi mitatu ijayo. Ninasubiri kwa hamu siku itakapotangazwa kwamba kama sehemu moja ya kujizatiti, kila tawi la Benki linafunga mahesabu yake kila siku. Ili kutimiza wajibu wake barabara Benki ya Taifa ya Biashara inahitaji ushirikiano mkubwa kutoka kwa wateja wake, ikiwa ni pamoja na Mashirika ya Umma na hasa Mamlaka za Mazao. Mwisho

nimehakikishiwa kuwa Benki inaandaa mipango thabiti ya mafunzo kwa ajili ya watumishi wake ili kuongeza uwezo wao na kufanikisha mfumo mpya wa mgawanyo wa madaraka kati ya makao makuu na mikoa.

**Benki ya Maendeleo Vijijini:**

24. Hivi sasa Kamati maalum chini ya uongozi wa Benki Kuu ikishirikiana na Idara nyingine na hasa sekta ya Vyama vya Ushirika inaandaa mapendekezo maalum kwa madhumuni ya kuunda upya Benki ya Maendeleo Vijijini kwa madhumuni ya kuviwezesha vyama vya ushirika kutimiza wajibu wao katika kukuza kilimo na maendeleo vijijini. Hapo baadaye muswada utakao viwezesha vyama vya ushirika kushiriki katika uendeshaji wa Benki ya Maendeleo Vijijini utaletwa Bungeni ili utafakariwe na hatimaye upitishwe.

25. Ndugu Spika, ningependa kueleza kwamba kwa muda mrefu mahitaji mengi ya kilimo pamoja na maendeleo vijijini kwa ujumla yatategemea misaada na mikopo kutoka nje. Hii inatokana na ukweli kwamba mashine, zana, vyombo vya usafiri na pembejeo mbali mbali vitaendelea kununuliwa kutoka nje. Uwezo wa kupata vitu hivi kwa misaada au mikopo nafuu utategemea jinsi Benki itakavyofanikiwa kukusanya fedha inazokopesha wateja wake. Wafadhili na wakopeshaji wa nje wataendelea kutoa fedha ama kwa serikali au kwa dhamana ya serikali. Hii ina maana kwamba Benki ya Maendeleo Vijijini hata katika muundo wake mpya itawajibika kwa Bunge. Kwa hiyo, pamoja na kupanua shughuli za Benki hii, ikiwa ni pamoja na kuvishirikisha Vyama vya Ushirika ni lazima tusaidie Benki hii kuimarisha shughuli zake kwa kuhakikisha kwamba mikopo iliyotolewa na Benki inalipwa kwa wakati wake. Maendeleo ya kilimo pamoja na maendeleo vijijini yatategemea sana juhudi hizi.

**Benki ya Raslimali:**

26. Hali ngumu ya uchumi imeathiri shughuli za Benki ya Raslimali. Kwa kuwa wateja wengi wa Benki ni viwanda ambavyo vina matatizo ya kutoweza kutumia uwezo wao wa

uzalishaji kikamilifu, hali ya Benki ni vizuri ileweke katika mazingira haya. Serikali inahimiza Benki iendelee kutafuta misaada kutoka nje kwa njia ya mikopo kupata malighafi ya kuviwezesha viwanda vilivyopo vifanye kazi kwa uwezo wao.

**Benki ya Nyumba:**

27. Ndugu Spika, katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka jana nilieleza matatizo yaliyokuwa yanakabili Benki ya Nyumba. Tatizo mojawapo kubwa lilikuwa ni ukosefu wa wataalam wenye uzoefu wa kutosha. Niliitaja pia kwamba Tume maalum ilikuwa imeteuliwa ili kushughulikia matatizo hayo na kutoa ushauri. Vile vile nilieleza kwamba mapendekezo ya Tume maalum yalikubaliwa na Wizara yangu na kwamba hatua za utekelezaji zilichukuliwa na Benki. Benki imeendelea kuyatekeleza mapendekezo hayo ikiwa ni pamoja na matumizi ya vijitabu vya miongozo ya taratibu mpya za utoaji fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba. Benki pia imeendelea kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wake waliopo kuhusu utaratibu huo mpya. Zaidi ya hayo Benki imeimarisha shughuli zake kwa kuajiri wafanyakazi wapya wenye ujuzi katika fani mbali mbali. Mahesabu ya mwaka 1980 yamekaguliwa na hesabu za mwaka 1981 zinaendelea kukamilishwa.

**Shirika la Bima la Taifa:**

28. Kwa ujumla maendeleo ya Shirika hili yamekuwa ya kuridhisha. Kwa wakati huu uwezo wa Shirika wa kuendelea kutoa huduma umekwamishwa na hali mbaya ya fedha za kigeni ambayo imelifanya lisiweze kurejesha malipo kwa makampuni ya Bima ya nchi za nje. Serikali inafanya kila juhudi kutatua tatizo hili. Vile vile uongozi wa Shirika umetakiwa kuongeza juhudi katika kupunguza gharama za uendeshaji ambazo zinaonekana kuongezeka kwa kiasi kikubwa.

**Kampuni ya Tanganyika ya Fedha za Maendeleo—TDFL:**

29. Ndugu Spika, matatizo ya uchumi yaliyokabili Mashirika mengine ya Fedha mwaka 1981 pia yalikuwa na athari hizo kwa Shirika hili. Kwa mara ya kwanza tangu Shirika lianze, shughuli za utoaji mikopo kwa miradi mipya

zilipungua kuliko miaka mingine yote. Hata hivyo pamoja na matatizo haya, Shirika hili lilijitahidi kuidhinisha mikopo yenye thamani ya Sh. 34.3 milioni kwa ajili ya miradi mitano. Kiasi cha fedha kilichotolewa kutokana na mikopo iliyoidhinishwa na Shirika kwa ajili ya miradi mbali mbali mwaka wa 1981 kilikuwa Sh. 25.1 milioni ukilinganisha na Sh. 57.2 milioni zilizotolewa mwaka 1980. Kupungua kwa kiwango hiki cha fedha zilizotolewa kwa asilimia 56 kumetokana na uchelewaji katika utekelezaji wa miradi ambayo ilishaidhinishwa hapo awali.

**Benki ya Posta:**

30. Ndugu Spika, mwaka 1981 ulikuwa ni mwaka wenye mafanikio madogo. Kutokana na hali ngumu ya uchumi nchini wateja wengi wa Benki hii walipunguza uwekaji wa akiba. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 1981 jumla ya thamani za amana katika Benki ilikuwa shilingi 275·6 milioni. Inatarajiwa kuwa itakapofika mwisho wa mwaka huu wa fedha jumla ya amana itakuwa shilingi 278·7 milioni. Hili ni ongezeko la shilingi 23·1 milioni ukilinganisha na ongezeko la shilingi 31 milioni kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 1980. Hadi kufikia mwishoni mwa 1981/82 Benki hii inatarajia kununua dhamana za Serikali zenye thamani ya shilingi 45 milioni ukilinganisha na dhamana za shilingi 55 milioni zilizonunuliwa mwishoni mwa 1980/81. Katika mwaka 1982/83 Shirika linategemea kwamba thamani ya amana za wateja itaongezeka kwa shilingi 44·5 milioni kutoka shilingi 298·7 milioni hadi kufikia shilingi 343·2 milioni itakapofika tarehe 30 Juni 1983.

**Shirika la Taifa la Ukaguzi:**

31. Ndugu Spika, kwa kipindi cha mwaka 1980/81 Shirika la Ukaguzi wa Hesabu lilikagua na kudhibiti Hesabu 282 za mashirika 220 ya Umma. Hii ni ongezeko la asilimia 18 ikilinganishwa na Hesabu 239 za mashirika 200 zilizokaguliwa kwa mwaka uliotangulia. Hesabu 149 zilikuwa katika hatua mbali mbali za ukaguzi. Mashirika mengine yalikuwa yameleta Hesabu za miaka hadi mitano

kwa pamoja. Mashirika 137 na vyama 14 vilivyoshirikishwa na Baraza la Michezo la Taifa hayakuweza kuwasilisha Hesabu zao kwa ukaguzi hata baada ya mwaka kupita tangu mwaka wa fedha ulipoisha.

32. Kati ya Hesabu 282 zilizokaguliwa, Hesabu 85 zilipata hati safi za ukaguzi, Hesabu 138 zilipata hati za ukaguzi wenye dosari, Hesabu 43 zilipata hati za ukaguzi mbaya na Mkaguzi hakuweza kutoa maoni yoyote kuhusu Hesabu 16. Kati ya hesabu 282 zilizokaguliwa, Hesabu 117 zilionyesha faida yaani mapato yalizidi matumizi, Hesabu 110 zilionyesha hasara yaani matumizi yalizidi mapato, na Hesabu 55 hazikuonyesha faida au hasara kwa sababu Mashirika yanayohusika yalikuwa bado hayajaanza kuzalisha mali au kutoa huduma, au fedha iliyohusika ilikuwa ya Mifuko iliyotengwa kwa madhumuni maalum.

33. Ndugu Spika, katika hotuba yangu ya mwaka jana nilitaja kasoro mbali mbali zinazoathiri ufuatiliaji mzuri wa kutekeleza mapendekezo yanayotolewa na Shirika la Ukaguzi baada ya kukagua Shirika linalohusika. Kasoro hizi kama zinavyoelezwa mara kwa mara ni pamoja na uendeshaji dhaifu wa mashirika, baadhi ya Bodi za Wakurugenzi hazitimizi wajibu wao, usimamizi mdogo wa Wizara Mama, ukosefu wa Idara za Ukaguzi wa Ndani (Internal Audit) katika mashirika kadhaa, n.k. Matatizo haya bado yangali yapo katika mashirika mengi na ni wajibu wa kila Shirika na Wizara Mama kuhakikisha kwamba maoni ya wakaguzi yanatekelezwa. Vinginevyo lengo letu kutaka kuhakikisha kuwa mahesabu ya mashirika yanawekwa sawa litakuwa halina maana. Ndugu Spika, ningependa kufahamisha Bunge lako tukufu kwamba Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma kwa mwaka uliopita imefanya kazi yake vizuri na ni matumaini yangu kuwa kazi hii nzuri itaendelezwa mwakani ili wale wote wanaokiuka misingi ya mahesabu wachukuliwe hatua zinazostahili.

**Shirika la Bahati Nasibu ya Taifa:**

34. Ndugu Spika, katika mwaka uliopita Shirika hili liliendelea na shughuli zake vizuri. Katika hotuba ya mwaka jana nilitaja kuwa Shirika hili lilikuwa linatarajia kufungua

ofisi za kanda huko Dodoma na Mtwara. Kutokana na hali ngumu ya uchumi mpango huu umeahirishwa mpaka hapo hali itakaporuhusu. Ndugu Spika, pamoja na kuwa hatukuweza kufungua ofisi hizi za kanda, hata hivyo nafurahi kusema kuwa mauzo ya tikiti za Bahati Nasibu yalikuwa ya kuridhisha, na hata kuvuka lengo lililowekwa. Katika mwaka 1981/82 tikiti 1,811,002 ziliuzwa ukilinganisha na tikiti 1,740,000 zilizouzwa mwaka 1980/81. Hili lilikuwa ni ongezeko la asilimia 4.

**Shirika la Akiba ya Wafanyakazi la Taifa:**

35. Ndugu Spika, idadi ya wanachama katika Shirika la Akiba ya Wafanyakazi la Taifa iliongezeka kwa asilimia 9.4 na kufikia 350,000 kwa mwaka 1981/82. Ingawa Shirika lilifanikiwa kukusanya kiasi cha Sh. 175 milioni kwa kipindi cha kati ya Julai, 1981 na Machi, 1982 ambacho ni asilimia 45 ya makadirio ya Sh. 395 milioni ya mwaka mzima nimehakikishiwa kuwa kuna uwezekano wa kufikia lengo lililokadiriwa. Kuhusu ununuzi wa dhamana za Serikali ninafurahi kutamka kwamba Shirika limeshanunua dhamana zenye thamani ya Sh. 272 milioni kati ya dhamana zenye thamani ya Sh. 280 milioni zilizokusudiwa. Shirika limeendelea kuongeza ufanisi katika kazi na juhudi zinafanywa ili kuimarisha viwango vya ujuzi wa wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo mbali mbali.

36. Ndugu Spika, ningependa kuwashauri Ndugu Wabunge wapitie majedwali mbali mbali yaliyoambatishwa kwenye hotuba hii.

**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu:**

37. Hali ya ukaguzi wa hesabu kwa mwaka 1980/81 haijabadilika sana ikilinganishwa na mwaka 1979/80. Kumeendelea kuwa na ucheleweshaji wa kuwasilisha hesabu kwa ukaguzi na hivyo hali hii imesababisha Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ichelewe pia. Kati ya hesabu za Wizara thelathini na nne, 21 zilipewa hati safi za ukaguzi, 3 zilipewa hati za kuridhisha na zilizobakia hesabu

zao hazikukubalika. Kwa upande wa mikoa ni miwili tu ndio iliyopata hati safi. Tukilinganisha na miaka mitano iliyopita yaani kwa mwaka 1975/76 hali ya ukaguzi wa hesabu ilikuwa kama ifuatavyo: Wizara 15 zilipata hati safi; Wizara saba zilipewa hati za kuridhisha na kwa upande wa mikoani minne tu iliyopata hati safi. Kama inavyoonekana, Ndugu Spika, hali hii haiwezi kuendelea hivyo. Ni matumaini yangu kwamba kadri tunavyoendeleza mafunzo ya wahasibu wa ngazi mbali mbali katika vyuo vya hapa nchini na nje ndivyo hali ya uhasibu Serikali itakuwvozidi kuimarika.

**Mafunzo ya Uhasibu:**

38. Ndugu Spika, Ndugu Wabunge wanafahamu uhaba mkubwa wa wahasibu wa ngazi zote uliopo nchini. Tukiwa tunajiandaa kuanzisha Serikali za Mitaa na Vyama vya Ushirika ni dhahiri kwamba mahitaji ya wahasibu waliohitimu yataongezeka kwa kiasi kikubwa na hivyo kukuza uhaba uliopo na hasa tukizingatia idadi ndogo ya wahasibu wanaofuzu kila mwaka. Napenda kuwashukuru Ndugu Wabunge watano ambao wametumia muda wao katika kuchunguza kwa undani hali halisi ya tatizo hili na natege mea, hapo baadaye, kupata taarifa yao kamili. Napenda vile vile kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu itashughulikia mapendekezo ya taarifa itakayotolewa kwa kadri ya uwezo wetu. Ninaamini kwamba Idara zote za Serikali, Vyama vya Ushirika, Mashirika ya Umma, Jumuiya ya Wafanyakazi na Serikali za Mitaa watatoa mchango wao kikamilifu katika kutekeleza mapendekezo yatakayotokana na taarifa hii ambayo inahusu suala muhimu kitaifa.

## MASHIRIKA YA KIMATAIFA NA YA KANDA

**Benki ya Maendeleo ya Afrika ya Mashariki:**

39. Ndugu Spika, inaonekana kwamba chini ya uongozi thabiti wa Mkurugenzi Mkuu na usimamizi bora wa Bodi ya Wakurugenzi, Benki ya Maendeleo ya Afrika ya Mashariki

inaweka msingi ambao utatuwezesha kukuza ushirikiano baina ya nchi za Afrika ya Mashariki katika maendeleo ya viwanda hasa kwa wakati ule ambao hali ya uchumi duniani itarubusu.

**Benki ya Maendeleo ya Afrika:**

40. Ndugu Spika, Ndugu Wabunge watakuwa na taarifa kuwa katika mkutano wa hivi karibuni wa mwaka wa Bodi ya Magavana na Benki hii uliofanyika Lusaka, uamuzi wa kuruhusu nchi zisizo wanachama kununua hisa za Benki ulipata asilimia 75 ya kura zote wakati Nigeria ilipounga mkono uamuzi huu baada ya kutafakari suala hili kwa muda wa miaka miwili. Hii inamaanisha kuwa Benki sasa itakuwa na mtaji mkubwa zaidi katika miaka mitatu ijayo kwa ajili ya kutoa mikopo katika nchi za Kiafrika. Wakati huo huo ni muhimu kabisa kwa Benki kujikumbusha kwamba mahitaji mubimu ya nchi za Kiafrika ni pamoja na uanzishaji wa miradi inayosaidia kuendeleza uchumi, maendeleo ya kilimo vijijini na mafunzo ya wataalam. Vitu hivi vyote huchukua muda kabla matunda yake hayajaonekana kiuchumi.

41. Ndugu Spika, hivi karibuni Serikali imekuwa na mazungumzo na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kufuatana na matakwa ya kifungu cha IV cha Katiba iliyoanzisha Shirika hilo. Kwa kawaida, mazungumzo ya aina hii hufanyika kila baada ya miaka miwili au mitatu ili kuliwezesha Shirika hilo kupima na kuelewa hali ya uchumi, na kufahamu sera ya fedha ya nchi ambazo ni wanachama wake. Ni matumaini yangu kwamba taarifa itakayotolewa na ujumbe uliokuja kwa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika hilo itazingatia mpango wa Serikali wa kurekebisha hali ya uchumi wetu.

42. Serikali inatambua wazi kwamba uzalishaji wa mazao ya biashara yanayouzwa nje unategemea mambo kadhaa. Hali ya hewa, upatikanaji wa mbegu bora, zana na pembejeo, barabara kuu na ndogo zinazopitika wakati wowote, usafiri mzuri na hifadhi bora ya mazao, usimamizi thabiti katika ununuzi, usindikaji, usambazaji na uuzaji kwenye masoko ya nje, upatikanaji wa bidhaa muhimu madukani na bei zenye

kutoa motisha kwa wakulima kwa mazao mbali mbali. Ni dhahiri kwamba kila moja au yote haya kwa pamoja yanahusika katika kufanikisha shughuli za kilimo. Ni dhahiri pia kuwa mambo yote haya yanahitaji mtaji mkubwa na watu wenye ujuzi wa shughuli hizi.

43. Ndugu Spika, katika tofauti za maendeleo zilizopo kati ya nchi tajiri na nchi maskini, ambazo umaskini wake unatokana na miaka mingi ya kukandamizwa, jumuia ya mataifa haijakubaliana juu ya mfumo ambao utawezesha nchi tajiri kuchangia maendeleo ya nchi maskini. Vile vile haielekei kama mfumo huu uko karibu kufikiriwa. Hadi wakati huo, itabidi nchi maskini ziendelee kupambana na hali mbaya ya uchumi na mfumo mbaya wa biashara duniani na katika hali hii wanyonge watazidi kuwa wanyonge zaidi.

44. Katika hali hii tunalazimika sisi wenyewe kubeba mzigo huu wa maendeleo. Hata hivyo natarajia kuwa nchi rafiki na mashirika ya Kimataifa ikiwa ni pamoja na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia, wataendelea kutusaidia kadiri ya uwezo wao, katika kutupunguzia mzigo huu mzito tulioubeba ili lengo la.muda mrefu la kuleta maendeleo na amani kwa mataifa yote lifikiwe. Nchi zinazoendelea kama Tanzania, ambazo katika mfumo wa maendeleo duniani ni nchi za pembezoni zinalazimika kujibanza na nchi za kiini. Hali hii ambayo si ya kuridhisha inahitaji kueleweka na nchi zilizoendelea na kutafutiwa ufumbuzi wa kudumu.

45. Kuendelea kuwepo kwa hali ngumu ya uchumi duniani kunafanya hali ya uchumi wa nchi nyingi za Kiafrika iendelee kuwa ya hatari zaidi. Hadi tarehe 31.3.82 jumla ya akiba ya fedha za kigeni ya nchi zote zinazoendelea ambazo hazina mafuta ilikuwa Dola za Marekani 65,543 milioni. Kati ya hizi dola 13,800 milioni ni mkopo kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF). Dola 51,743 milioni zilizosalia ndio akiba yao halisi ya fedha za kigeni. Wakati huo huo akiba ya fedha za kigeni ya nchi zote za Kiafrika zisizo na mafuta ilikuwa dola 3,283 milioni, na kiasi hicho ni baada ya kupata mkopo wa dola 3,562 milioni kutoka IMF na hivyo kuwa

pengo halisi la dola 279 milioni. Jumuia ya Kimataifa inawajibika kuielewa hali hii ngumu ya uchumi inayozikabili nchi za Kiafrika ambazo hazina mafuta, na kuchukua hatua zinazofaa zenye madhumuni ya kurekebisha hali hii.

46. Ndugu Spika, kwa mara nyingine tena napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa niaba ya Serikali kwa nchi zote marafiki pamoja na mashirika mbali mbali ya fedha na maendeleo kwa misaada yao ambayo tumeipata katika wakati huu mgumu. Vile vile tunatoa shukurani kwa Serikali za nchi mbali mbali kwa misaada waliyotupa na pia kwa Mpango wa Chakula Duniani (WFP) kutupatia chakula ambacho tunakihitaji kutokana na ukame ulioikumba mikoa mingi mwaka jana. Wakati huo huo ningetoa masikitiko yangu kwa kushindwa kwa Shirika la Maendeleo la Kimataifa (IDA) kupata mtaji wa kutosha kutokana na msimamo uliochukuliwa na Serikali ya Marekani. IDA imesaidia nchi zinazoendelea kwa muda wa zaidi ya miaka ishirini. Hivi leo kuna hatari ya mafanikio haya yote kupoteza maana ijapokuwa mzigo ambao nchi zinazoendelea zinalazimika kubeba unazidi kuwa mzito.

**Makadirio ya Matumizi na Mapato 1982—83:**

47. Ndugu Spika, sasa nitazungumzia makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika mwaka 1982-1983, ambayo yanazingatia maelezo ya mpango wa kurekebisha hali ya uchumi ambao unasisitiza uimarishaji na ubanaji wa matumizi ya Serikali.

48. Matumizi ya kawaida ya Serikali yamekadiriwa kuwa shilingi 14,144·0 milioni ikilinganishwa na mategemeo ya matumizi halisi katika mwaka huu ya shilingi 13,687 milioni na makadirio ya bajeti ya shilingi 12,205·4 milioni. Sehemu kubwa ya ongezeko la matumizi imetokea katika Huduma za Mfuko Mkuu na limesababishwa na malipo ya mikopo ya Serikali kutoka mabenki yetu na ya mkopo wa ujenzi wa Reli ya TAZARA uliotolewa na Jamhuri ya Watu wa China.

49. Kuhusu Mapato, tukizingatia pengo la Shilingi 221 milioni mwaka huu, makisio ya ukusanyaji wa kodi ya mapato, na bila kubadili viwango vya kodi, ni jambo la busara kukadiria mapato ya shilingi 10,700 milioni yakilinganishwa na mategemeo ya shilingi 10,460 milioni katika mwaka huu. Makisio haya yako katika misingi ya kuzingatia viwango vya sasa vya kodi.

50. Ndugu Spika, mgawanyo wa matumizi ya kawaida ni kama ifuatavyo:—

| | Sh. |
|---|---|
| Mfuko Mkuu ............................................ | 2,328m |
| Wizara .................................................... | 6,244m |
| Mikoa ..................................................... | 3,199m |
| Ruzuku .................................................... | 1,102m |
| Uimarishaji Mashirika ya Umma .............. | 730m |
| Matumizi maalum pamoja na ya Dharura, gharama za uendeshaji zitakazotokana na miradi itakayokamilika ...................... | 541m |

51. Ndugu Spika, itakumbukwa kuwa mwaka jana niliwasihi wanaohusika juu ya umuhimu wa Idara za Serikali kuzingatia viwango vya fedha vilivyoidhinishwa na Bunge. Nilisema hali ya mapato yetu ilitegemea sana mazingira yetu. Hivyo inatubidi kudbibiti matumizi ili kulinda uchumi wetu kutokana na athari mbaya za ongezeko kubwa sana la bei. Mwaka huu hatukumudu vizuri kuthibiti matumizi yetu, hivyo hali hii imesababisha ongezeko kubwa la bei. Kwa vile mwaka huu hali ya mapato ni ngumu zaidi, suala la Idara zote za Serikali kuzingatia viwango vya matumizi ambavyo vitaidhinishwa na Bunge, ni suala la kufa na kupona kwa kuwa Serikali ni Idara zote.

52. Ndugu Spika, wakati wa kutayarisha bajeti, uamuzi wa kuweka kiwango cha kukopa kutoka kwenye mabenki kiasi cha Sh. 4,376 milioni ulifanyika baada ya mashauriano marefu. Hiki siyo kiwango ambacho kimefikiwa kwa urahisi. Hii ni hatua ambayo italeta ongezeko la bei na lazima usimamizi wake uwe wa uangalifu sana.

53. Ndugu Waziri wa Mipango na Uchumi amekwishaeleza kwa kinaganaga hali ambayo imefanya Serikali kufanya uamuzi wa kupunguza matumizi ya Maendeleo. Ningependa tu kuwakumbusha Ndugu Wabunge kwamba tatizo linalotukabili siyo tu upungufu wa fedha za kigeni na ukosefu wa wataalam bali pia ni kwamba uwezo wetu wa kubeba mzigo wa matumizi ya kawaida yatokanayo na miradi ambayo imeshakamilika ni mdogo sana. Ukweli ni kwamba kwa kipindi cha miaka michache ijayo hatutakuwa na uwezo huo. Matumizi ya kawaida ya sasa ni matokeo ya jumla ya maamuzi tuliyofanya hapo awali kuhusu uendelezaji wa miradi. Matumizi haya yana gharama kubwa kwa upande wa fedha za kigeni.

54. Ndugu Spika, hatua moja ambayo itapunguza mapato ya Serikali nitaitangaza leo. Tokea leo Serikali imeamua kuondoa kodi ya kusafirishia bidhaa nje kwenye zao la pamba. Imeonekana hakuna sababu ya kukusanya kodi hii ambayo hutozwa kwa kiasi cha Sh. 2/10 kwa kilo moja ya pamba iliyochambuliwa na wakati huo huo kutoa ruzuku kubwa zaidi kwa Mamlaka ya Pamba ili kufikia gharama ya bei iliyopangwa kumlipa mkulima katika mwaka huo. Sina shaka Ndugu Wabunge watakubaliana nami kwamba Mamlaka ya Pamba inalo jukumu la kipekee la kupunguza gharama zake ili kupunguza mahitaji ya ruzuku kutoka Serikalini ambayo kwa sasa ni kubwa mno. Ruzuku za aina hii zinambebesha mlipa kodi mzigo ambao hastahili kuubeba na wakati huo huo zinasababisha ongezeko la bei wakati ambapo hali ya uchumi inazidi kuwa ngumu.

55. Utaratibu wa kukusanya mapato ya Serikali unaendelea kutazamwa upya na marekebisho yatafanywa yenye madhumuni ya kuongeza ufanisi. Hivi sasa kuna sehemu mbili ambako kuna udhaifu ambao unahitaji kurekebishwa. Kwanza ni kuhusu Hati za misamaha ya kodi ambazo hutolewa kwa ajili ya kununulia malighafi (Registered Dealer's Certificates). Katika kudhibiti ulipaji wa kodi ya mauzo imedhihirika kwamba baadhi ya viwanda vimekuwa vikikwepa kutimiza wajibu wao wa kulipa kodi inayostahili kulipwa. Kwa kawaida hati hizi hutolewa kwa

wale ambao hutumia malighafi ambazo hutozwa kodi ya mauzo. Ili kuhakikisha kwamba kodi inatozwa kwa bidhaa zenye thamani kubwa, kwa mfano mavazi, mtengenezaji mavazi huruhusiwa kununua malighafi bila kutozwa kodi na baadaye hutozwa kodi kwenye mavazi anayotengeneza. Baada ya kuonekana kwamba usimamiaji wa masharti yanayoambatana na misamaha inayotolewa chini ya utaratibu huu umekuwa mgumu na ili kuziba mwanya wa kukwepa kulipa kodi; imeamuliwa kufanya uchambuzi wa kila kiwanda kilichopewa Hati ya "RDC" lengo likiwa kuhakikisha kwamba ni wale tu watakaothibitika kwamba wanalipa kodi hiyo kwa ukamilifu kama ilivyokusudiwa na sheria ndio watakaoruhusiwa kuendelea kutumia hati hizo.

56. Hatua nyingine ni ya kiutawala. Imejengwa tabia ya kuwasamehe Ushuru wa Forodha na Kodi ya Mauzo makondrata wanaojenga miradi inayogharimiwa na Serikali na Mashirika ya Umma kwa fedha za misaada na mikopo kutoka nje. Msingi wa utaratibu huu ni mawazo ya kwamba kwa sababu miradi hii inagharamiwa na Serikali na Mashirika ya Umma, Serikali ijiepushe na ukusanyaji kodi ambao utaongeza gharama za miradi hiyo. Uchunguzi umedhihirisha kwamba ni vigumu kwa kondrata kuorodhesha bidhaa zote anazotegemea kutumia kwa kila mradi. Hali hii imesababisha bidhaa zilizoingizwa zaidi ya zile zinazotumika katika miradi ya Serikali na Mashirika ya Umma kutotozwa kodi. Kwa hiyo imeamuliwa kwamba ni kwa manufaa ya taifa, vifaa na zana za miradi hiyo vitozwe ushuru wa forodha na kodi ya mauzo ili kuziba mwanya uliopo.

57. Ndugu Spika, Serikali imeamua kwamba haitakuwa kwa manufaa ya umma kubadilisha viwango vya kodi mwaka huu isipokuwa kodi ya mauzo ya pamba imeondolewa. Hatua mbali mbali zinazotumika hivi sasa za kukusanya kodi zitaimarishwa. Hivi sasa tayari kumekuwepo na hali ya kuridhisha katika makusanyo ya kodi ya mapato. Sote tunatambua kuwa kodi ya mapato inatokana na mapato. Kwa wakati huu walipaji kodi wote kwa jumla wanakabiliwa na hali ngumu ya uchumi. Hata hivyo, nitakuwa mtu wa

kwanza kukiri kwamba kuna watu binafsi na familia zao ambao wanayo mapato makubwa lakini hayatozwi kodi. Ingawa tunakabiliwa na upungufu wa wafanyakazi wenye uznefu wa kukusanya kodi, upungufu wa vyombo vya usafiri n.k. tutaendelea kuongeza juhudi zetu za kukusanya kodi. Wote hao ambao wanakiuka sheria ya kulipa kodi watakaposhikwa, wataadhibiwa vikali.

58. Kwa upande wa matumizi ya serikali itabidi kila Afisa Mwajibika wa Wizara, Idara na Mikoa asimamie moja kwa moja maafisa walio chini yake na kuhakikisha kwamba hundi za malipo haziandikwi ikiwa fedha haipo. Tukizingatia nidhamu hii hakuna sababu ya kutufanya tuvuke viwango vilivyoidhinishwa katika kasma zetu. Wahasibu wote wameagizwa kumuarifu Katibu Mkuu wa Hazina mara mtu ye yote anapomlazimisha mhasibu huyo kuandika hundi zinazozidi fedha zilizopo. Hatua za kinidhamu zitachukuliwa haraka dhidi ya maofisa wanaohusika. Hii ndiyo hali ya vita ambayo sasa tunakabiliana nayo. Katika hali hii, Wizara Mama zinategemewa vile vile kufuatilia kikamilifu matumizi ya mashirika yaliyoko chini yao.

59. Ndugu Spika, ningependa kunukuu maneno yafuatayo kutoka kwenye hotuba ya Rais Reagan alipowasilisha mapendekezo ya Bajeti Bungeni kwao "Nakisi (deficits) tunazozipendekeza ni kubwa mno kuliko ambavyo tungelipendelea. Lakini hili ni ovu la lazima katika dunia halisi ya leo".

60. Ndugu Spika, nakisi ambayo utawala huo wa Marekani ulipendekeza na ambayo waliiona kuwa ni kubwa mno kuliko ambavyo wangependelea ni asilimia mbili na nusu ya Pato la Taifa (G.N.P.) la Marekani. Mikopo tunayoipendekeza kutoka katika mabenki yetu ni asilimia zaidi ya 10 ya Pato la Taifa (G.N.P.). Ikiwa Marekani inadiriki kuchukua hatua hii na sote tunajua ni nini maana ya nakisi hiyo kwetu hasa athari yake katika masoko ya fedha, kupanda kwa riba, na uhusiano wa thamani za sarafu duniani, ni dhahiri kwamba Tanzania hatutamudu kuutwisha uchumi wetu mdogo mzigo ambao ni zaidi ya mara nne ya kiwango hicho cha Marekani.

61. Ninalotaka kufafanua kwa kutumia tarakimu hizo ni kwamba haitakuwa na manufaa kwa uchumi wa taifa iwapo ongezeko la karadha haliwakilishi kiwango cha uzalishaji mali kinachotosheleza mahitaji ya kawaida na ziada ya kuwekeza katika uimarishaji na upanuzi wa uchumi. Hili ndilo hasa lengo letu. Kinyume na shabaha hiyo bado tunalazimika kuendelea kutumia kiasi kikubwa zaidi kuzidi kile tunachozalisha ama kwa kukopa au kwa kutegemea misaada tunayopata kutoka nje.

62. Mpango wa kurekebisha hali ya uchumi utakuwa umetusaidia iwapo katika kipindi cha miaka mitano ijayo tutakuwa tumefikia kiwango cha uzalishaji kinachotosheleza matumizi yetu na kubakiwa na ziada ya kuwekeza vitegauchumi. Mahitaji ya shule, hospitali, barabara, usalama, utawala, sheria na amani ni baadhi ya matumizi ya ujumla ya kijamii ambayo budi yajumlishwe na matumizi ya kila mmoja wetu ya chakula, nyumba, nguo, n.k. katika kufikia jumla ya matumizi ya taifa. Hivyo uzalishaji ni lazima uwe katika kiwango kinachozidi matumizi haya ili tuweze kuwa na ziada ambayo itawekezwa na kuongezeka iweze kuvinufaisha vizazi vijavyo. Pamoja na kuelemewa na hali mbaya ya uchumi duniani hatuna budi kujizatiti mara moja na kuchukua hatua za kurekebisha hali ya uchumi wetu bila kuzidi kuchelewa.

63. Ndugu Spika, napenda sasa kuchukua nafasi hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa Chama cha Mapinduzi kwa uongozi wake imara wakati huu wa hali ngumu ya uchumi wetu. Napenda pia kutoa shukurani zangu kwa Kamati ya Bunge ya Fedha za Serikali, Kamati ya Bunge ya Fedha na Mipango, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma, Mhasibu Mkuu wa Serikali, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa mchango wao muhimu katika kuthibiti usimamizi wa fedha zetu. Zaidi ya haya napenda kuzishukuru Idara zote za Serikali kwa mchango wao katika kushughulikia masuala mengi magumu na hivyo kuwezesha utayarishaji wa bajeti hii ufanikiwe.